ALL RIGHTS RESERVED
(First Edition)

Lazima tusisahau kamwe kuwa, imani ya kweli na tabia zuri, lazima iende pamoja kila siku, na hiyo tabia zuri uinuka kutokana na imani ya kweli. Mungu ufurahishwa na mienendo yetu katika maisha, ikiwa tu itainuka kutoka kwa uaminifu katika Yeye na Neno lake.

(We must never forget that right belief and right behaviour must always go together, and that right behaviour arises from right belief. God is pleased with our conduct in life only when it arises from trust in Him and His word.)

# "Heshima Zote kwa Mungu"
# ("All Honour to God")

Apostle Cliff Flor

Apostolic Church of Queensland - Northern District

P.O. Box 8077

Mt. Pleasant Q 4740

AUSTRALIA

Rev. Daniel M. Asiago

Unity Apostles Church

P.O. Box 334

Ogembo - 40204

KENYA

Translation Assistance

Evangelist Ronald Omanga

Unity Apostles Church

KENYA

# YALIYOMO (Index)


Ukurasa
(Page)

Kanuni ya imani ya kanisa la Mitume....................................................3-4
(The tenets and faith of the Apostolic Church)
Amri kumi za Mungu zilizopewa Musa katika mlima wa Sinai (Kutoka 20).............. 5
(The Ten Commandments as God gave to Moses on Mt. Sinai (Exo. 20)
Amri zilizonenwa na Yesu kama iliyoandikwa katika Mariko Mtakatifu 12............. 6
(The Commandments as spoken by Jesus as recorded in St. Mark 12)
Mafundisho ya Kidini (Religious teaching)................................................6-12
Maombi (Prayers)..........................................................................12-15
Maombi ya Bwana (The Lord's Prayer)....................................................13
Maombi ya watoto (Children's Prayers).............................................13-15
Maombi kwa watoto baada ya sara kwa chakula...................................13
(Prayer for the children after grace has been said for meals)
Maombi ya hasubuhi kwa watoto wadoga ......................................... 14
(Morning Prayer for little children)
Maombi ya jioni kwa watoto (Evening prayer for little children)..............14
Watoto baada ya Ushirika Mtakatifu (Children after Holy Communion).......14
Watoto wakiingia kanisani (Children entering Church)......................... 14
Maombi ya watoto kwa wa zazi wao walio wa mungu............................15
(A prayer for children for their Godly parents)
Tafsiri ya mfano wa 4H (Definition of the 4R emblem)....................................15
Maana ya Uthibitisho (The meaning of Confirmation)....................................16
Nyimbo za uthibitisho (Confirmation Hymns)....................................16-17
Uongozi katika maombi kwa washiriki (Guideline to prayers for members)........... 17
Maombi ya Asubuhi (Morning Prayer).............................................18
Salamu ya Asubuhi (Morning Salute)................................................18
Neema - Ombi mezani kabla ya kula mlo...........................................18
(Prayer at table before taking meals)
Maombi ya Jioni (Evening prayer)................................................... 19
Maombi mengine (Other prayers)....................................................20-21
Maombi kwa washiriki wakingia kwa ibada.......................................20
(Prayer for members entering for divine worship)
Maombi baada ya ushirika mtakatifu................................................ 20
(Prayer after partaking of the Lord's supper)
Maombi kwa wale walio gerezani kwa msamaha................................. 20
(Penitential prayer asking for forgiveness)
Maombi kwa furaha katika ndoa......................................................20
(A prayer for happiness in marriage)
Maombi ya kutuinua (A prayer to uplift us).......................................21
Baraka za Mtume (Apostle Blessing)................................................21

Catechism written in English............................................................ 23-42

# Kanuni ya imani ya kanisa la mitume

(The tenets and faith of the apostolic church in kiswahili language)

Hii kanuni na imani ilipatikana katika mafundisho ya mitume na neno la mungu lililopewa katika bibilia takatifu, kukiri imani kwa njia hii, lazima ifamike kwamba tunaamini kuna mungu mmoja tu, mungu aishiye na wa ukweli ambaye katika utatu wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, na, huu utatu ni mungu mmoja milele na milele.. Hii hujulikana kama fundisho la utatu wa mungu.

1. Tunamwamini mungu Baba, Mwenye nguvu zote, Muumba mbingu na nchi.
(Kumbukumbu la Torati 6:4, Wakorintho wa kwanza 8:4, Matayo 3:16-17, Matayo 28:19, Petro wa kwanza 1:2, Yohana wa kwanza 5:7)

2. Tunamwamini Yesu Kristo Mwana pekee wa Mungu Baba na Bwana na Mwokizi wetu, aliyezaliwa na bikra Maria, aliyekuwa mja mzitio kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; akateswa na akasulubiwa, akafa, akazikwa na akaingia mahali pa wafu, siku ya tatu akafufuka, aliwafundisha wanafunzi kwa siku arobaini (40) kuhusu ufalme wa Mungu, akapaa mbinguni kama mfalme mkuu, anakaa kwa mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi na atarudi tena kupokea waamini walio wateule wake, na katika siku ya hukumu atawahukumu walio hai na walio lala mauti.
(Mwanzo 1:31, Kutoka 20:11, Zaburi 102:25, Yohana 1:3, Waiberania 1:10, 11:3)

3. Tunamwamini Roho Mtkkatifu, Kanisa takatifu la mitume, ushirika mtakatifu, msamaha wa dhambi, kufufuliwa kwa wafu na uzima wa milele.
(Yohana 14:26, Petro wa kwanza 1:12, Waefeso 4:4-5, 4:13, 2:20, Wakorontho wa pili 13:14, Matendo 26:18, Luka 14:14, Ufunuo 20:6)

4. Tunaamini kwamba Bwana Yesu Kristo ni kichwa ya kanisa lake analolitawala na kulitunza kwa Roho Mtakatifu aliwatuma mitume na bado anawatuma mitume wake.
(Wakoloasai 1:18, Yohana 14:26, 6:63, Wakorintho wa pili 3:6, Matayo 28:18-20, Waefeso 2:20, Yoeli 2:23)

5. Tunaamini katika mtume kama mwalimu, msaidizi, mwombaji na balozi wa Bwana Yesu Kristo.
(Matayo 28:18-20, Matendo 26:17-18, Wakorintho wa pili 1:24, Timotheo ya kwanza 2:1, Wakorintho wa pili 5:20)

6. Tunaamini katika maandiko matakatifu, ya agano ya kale na agano jipya na ahadi zote ziko ndani kutoka mwanzo hadi mwisho.
(Isaiah 34:16, Warumi 15:4, Matayo 24:35, Petro wa kwanza 1:25, Timotheo wa pili 3:16)

7. Tunaamioni ubatizo mtakatifu wa maji tukiwa sehemu yake Yesu Kristo.
(Matayo 28:19, Wagalatia 3:27, Warumi 6:3-4, Yohana 13:8, Waefeso 5:26-27)

8. Tunaamini mwili na damu takatifu ya Yesu Kristo, kulingana na Sacrameni hii, kwamba Baba na mwana kwa Roho Mtakatifu wanaishi ndani yetu.
( Yohana 6:53-58, Wagalatia 2:20)

9. Tunaamini katika Mwili na Damu ya Yesu Kristo, nafsi zetu zikifunikwa na utakaso wake na kutayarishwa kwa arusi yake na kuwa chombo cha Roho Mtakatifu, ambaye Baba wa Mbinguni atufanya viumbe kama mwanaye aishiye milele.
(Mathayo 26:28, Ufunuo 7:9, 7:14, Warumi 8: 10, Ufunuo 21:2, Wakorintho wa kwanza 3:16, Yohana wa kwanza 2:29, Waefeso 4:13, Wakorintho wa kwanza 15:21-23)

10. Tunaamini katika kuwekwa wakfu wa kupokea upako wa Roho Mtakatifu, kuwekewa mikono ya mitume ili kufufua vipawa vya Roho Mtakatifu ndani yetu.
(Yohana 6:27, Matendo 10: 38, 8:17-18, Waefeso 1:13, Wakorintho wa pili 1:22)

11. Tunaamini kwamba Roho Mtakatifu hutupatia mafundisho yote kutoka mbinguni, kulingana na maneno na ahadi ya Bwana wetu Yesu Kristo kwa8 huduma wa mitume waliotumwa ulimwenguni kwa malengo haya.
(Johana 14:26, 15:16, 15:26-27, Mathayo 10:40, Luka 24:47-48, Ufunuo 21:14)

12. Tunaamini ya kuwa tunaishi siku za mwisho za Mungu (miaka elfu moja ni kama siku moja mbele za Mungu) na siku ile, Bwana Yesu atakaporudi, kupokea Bi arusi kwa wale waliolala mauti, na walio hai katika ufufuo wa kwanza.
(Kutoka 20:11, Petero wa pili 3:8, Mathayo 24: 30-31, Watesalonika wa kwanza 4:13-I8, Ufunuo 20:4-6)

13. Tunaamini katika umoja na Kristo mbinguni na baadaye, utakaso hutatimia duniani
(Yuda 14:15, Waefeso 5:26-27, Ufunuo 19:7-9, Waebrania 12:26, Petero wa pili 3:10)

14. Tunaamini katika utawala wa amani wa miaka elfu mioja duniani kama siku ya sabato ya Mungu, baadaye hukumu wa mwisho utekelezwe.
(Daniel 2:44, Mathayo 16:28, 25:34, Ufunuo 20:11-15)

15. Tunaamini katika Mungu Baba kama Muumba; katika Mwana wa Mungu kama kuhani mkuu anayetuombea, na katika Roho Mtakatifu katika ndani ya mwili na damu ya Yesu Kristo, kama mwalimu anayenena nasi katika kanisa takatifu la mitume.
(Nehemia 9:6, Waebrania 4:14-16, Warumi 8:9-14, Petero ya kwanza 3:18,1:15-19)

# Amri kumi za Mungu zilizopewa Musa katika mlima wa Sinai (Kutoka 20)

(The Ten Commandments as God gave to Moses on Mt. Sinai [Exo. 20]

1. Mimi ni Bwana wko niliyewatoa katika nchi ya Misri katika nyumba ya utumwa usiwe na miungu miingine ila mimi.

2. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia, isivisudie wala kuvitumia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; na wapatiliza wana maovu ya Baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami na waremu maelfu elfu wanipendao na kuzishika amri zangu.

3. Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana atamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

4. Ikumbuke siku ya sabato iutakase,. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato yake Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wko, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibariki siku ya sabato akaitakasa.

5. Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana Mungu wako.

6. Usiue.

7. Usizini.

8. Usiibe.

9. Usimsuchudie jirani yako uongo.

10. Usiitamanii nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe, punda wake, wala chochote alicho nacho jirani yako.

# Amri zilizonenwa na Yesu kama iliyoandikwa katika Mariko Mtakatifu 12

(The commandments as spoken by Jesus as recorded in St. Mark 12)

Ya kwanza ndio hii, sikia Israel, Bwana Mungu wetu ni Bwsana mmoja; naye mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndio hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine il'ryo kuu kuliko hizi.

# Mafundisho ya kidini

(Religious teaching)

1. Nchi na mbingu tunaiyona na wanyama, ndege, samaki, na mimea zilitokea wapi?
*Jibu:* Zote ziliumbwa na mungu kutoka pasipo kitu kwa neno lake la uwezo, katika siku sita katika wakati wake na kila kitu alichokifanya ikawa chema sana.
(Mwanzo l, waebrania 11:3, Neh 9:6, Ayubu 26:7, Zab 102:25, Matendo 14:15)

2. Ni sehemu gani muhimu sana katika uumbaji?
*Jibu:* wakati mungu aliumba mtu katika mfano wake, na kutokana mtu alimuumba mwanamke kama msaidizi wake.
(Mwanzo 1:26-27, Wakorosai 3:10)

3. Ina maana gani kwamba tulimbwa kwa mfano wa Mungu?
*Jibu:* Mungu yu sehemu tatu; Baba, mwana na roho mtakatifu na mtu aliumbwa na mwili, nafsi na roho katika njia hiyo.
(Mwanzo 2:7, Mat 10:28, 1 Wates 5:23, Yak 2:26)

4. Mbona mungu aliumba mtu wa kwanza, na kutokana na Adam mwanamke wa kwanza Hawa?
*Jibu:* Mungu alitaka mtu na mke wazae waongezeke, wakaijaze dunia na watu.
(Mwanzo 1:28, 1 Wakorintho 10:31, Zab 73:24, 2:26, Yoh 17:22-24)

5. Wale viumbe vilivyo juu je walifurahishwa na uumbaji wa mungu?
*Jibu:* La, shetani, mumalaika mkuu na wafuasi wake walifikiria kwamba wangekuwa ni wao wangeishi na mungu katika ufalme juu mbinguni.
(Mwanzo 3:13-15, Ufunuo 12:9-10, 20:2)

6. Ni agano ipi maalum mungu alifanya na adam na hawa katika siku zao za usoni?
*Jibu:* Mungu aliwahidi uzima wa milele kwa sharti kuwa watiifu, na wasile matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya ili wasije wakafa.
(Mwanzo 2:16-17, Meth 11:19, Ezek 18:4)

7. Je adam na hawa waliishi kwa hali waliyoumbwa?
*Jibu:* La, katika majaribu ya shetani hawakutii na walijaribu kujitetea na dhambi.
(Mwanzo 3:1-13)

8. Matokeo ya dhambi yalikuwa yapi?
*Jibu:* Ilimbidi mungu awafukuze kutoka shamba la edeni na akatangaza kifo cha mwili na akafanya mahali pa kuzimu kwa nafsi na kuongojea hukumu wa mwisho.
(Mwanzo 3:24, 3:19, Zab 16:10, Ufun 20:12-13)

9. Jinsi gani hii inatuhusu kwa vizazi vijavyo vilivyozaliwa na adam na hawa?
*Jibu*: Jinsi hii sisi zote tunaridhi uzima kutoka kwa adam na hawa sisi pia tukafikiwa na mauti kwa dhambi ya kwanza.
(warumi 5:12, 1 Wakorintho 15:22, Zab 51:5)

10. Hii ndio ilikuwa mwisho wa mpango wa mungu kwa mtu na mwanamke
*Jibu:* La, mungu habadiliki katika nyakati za mipango yake kutuma njia ulimwenguni kwamba mtu na mke wamrudie kama watoto wake kupokea ahadi zilizowekewa kwa mwanaadamu.
(Kutoka 3:14, Mal 3:6, Yak 1:17, Mwanzo 3:15)

11. Ni njia gani mungu aliongoza na kufundisha mwana adamu?
*Jibu:* Kwa miaka elfu nne (4000) mungu alionyesha nguvu zake, kwa gharika kuu, kutawanya watu katika babeli kwa kuwachagua watu na kuwaahidi nchi ya ahadi, kwa kutoa amri na dhabihu na kuwaongoza katika maneno ya wanabii lakini mwana adamu ameshindwa kushika ahadi za uzima wa milele kwa sababu ya dhambi.
(Mwanzo 6:7-8, 11:9, 17:19, Kutoka 14:29-30, 20, Mat 23:24, Mal 4:4-5)

12. Mungu alifanya nini ili kurudisha ahadi ya uzima wa milele kwa mwana adamu?
*Jibu:* Mungu alionyesha upendo wake kwa kumtuma mwanaye pekee Yesu Kristo kuwa mtu wa pili aliyeumbwa na mungu kushinda maadui wake dhambi, kuzimuni, mauti na kuanza njia mpya.
(1 Yoh 5:11, Yoh 1:1-14, Waeb 2:14, Luka 1:32, 2:1-15, Yoh 3:16)

13. Mtu wa pili aliumbwa kwa njia gani?
*Jibu:* Alitungwa mimba kwa njia ya roho mtakatifu na kuzaliwa na bikira na kwa njia hiyo akazaliwa na dhambi ya kwanza lakini alizaliwa na roho na mwili wa pili.
(Mat 1:23, Luka 1:26-35)

14. Kwa njia gani alimshinda adui dhambi?
*Jibu:* Yesu Kristo alishinda majaribu yote ya dhambi maishani mwake duniani, na bila dhambi, akachukua dhambi zote za ulimwengu kama dhabihu ya kweli.
(Mat 4:1-11, Yoh 1:29, waeb 4:15, 9:26, 1 Yoh 1:7)

15. Kwa njia gani alishinda adui kuzimuni?
*Jibu:* Baada ya kusulubiwa roho yake ilienda kuzimuni ikiwa ni njia ya kila mtu, lakini kwa sababu ya ushindi wake juu ya dhambi na uwaminifu wake kwa mungu, alikuwa na nguvu kushinda mauti na kuzimu milele na milele.
(Ufun 1:18, Luka 23:43, Waef 4:8-10, 1 Pte 3:19)

16. Alishinda adui mauti kwa njia gani?
*Jibu:* Katika siku ya tatu baada ya kifo chake Yesu Kristo alifufuka na mwili aonekane akiwa hai na wengi, kutuonyesha kwamba sasa mauti imeshindwa.
(Waeb 2:14, Luka 24:5-7, 24:39, Yoh 20:29, 1 Wakorintho 15:4-8)

17. Ni jukumu gani Yesu Kristo angetimiza?
*Jibu:* Yeye amewekwa kwa njia ya imani kila mwana adamu apate haki ya kurudi paradise kuishi katika ufalme wa mungu, na baadaye apate uzima wa milele katika utukufu wa mungu mbinguni.
(Waef 2:4-5, 1 Wakorintho 3:11, 1 Yoh 2:1, 1 Wakorintho 15:20-21)

18. Kwa njia gani haya yatafikiwa ulimwenguni?
*Jibu:* Bwana wetu alianza kanisa ambalo lingekuwa la kimataifa na la kimitume, akapaa mbinguni kuwa kichwa ya kanisa akituma roho mtakatifu kuongoza kanisa na kuwa mnabii na kuwa kuwani mkuu milele katika mkono wa kuume wa mungu kama mpatanishi kati ya mwana adamu na mungu hadi atumwe tena kudai kilicho chake na kuwa mfalme wa wafalme wetu.
(Yoh 20:21, 15:16, Matendo 1:8, 1:9, 2:1-4, Waef 5:23, 1 Tim 2:5, Waeb 6:20)

19. Jukumu na malengo ya kanisa ni yapi?
*Jibu:* Lengo la kanisa la mitume ni kuwaleta wote katika neema ya Yesu Kristo, kuunganisha watu na mungu tena na kuongozwa kama imani ya mtoto katika roho mtakatifu na kuandaliwa kama bi arusi wakati atarudi kwa nguvu na utukufu.
(Waef 2:4-5, 2 wakorintho 5:20, Yoh 16:13-14, Mat 24:31)

20. Tunapotesa nafasi yetu ndani ya kanisa, na ahadi zote, tukipita kutoka uzima huu?

*Jibu:* La, bwana wetu Yesu Kristo alishinda dhambi, kuzimu na mauti na kuwaandalia mahali kwa roho Ale zimejiandaa katika neema katika uzima hu, lakini kanisa litapaki na umoja na waumini wakiwa sehemu tatu.

(Yoh 14:1-4, Waarumi 14:8-9, 1:17, Ezek 41:16, 42:3-6)

21. Sehemu hii tatu ni ipi kulingana na neno la mungu?

*Jibu:* Kanisa lililo hai duniani chini ya dhahabu kwa wale waliouliwa, na paradise kwa wale roho zilizoitikia mwito wa bwana wetu Yesu Kristo.

(1 Pet 2:5, Ufu 6:9-11, Luka 23:43, waru 3:24-26, 2 wakorintho 12:9, Mat 16:24, 2 Wakorintho 12:4, Ufu 2:7)

22. Je mungu alikuwa na mpango kanisani jinsi ya kufanya kazi?

*Jibu:* Ndio mungu ni mungu wa mpango kutoka nyakati za mwanzoni kuonyesha kanisa lake lazima lifanye kazi kwa mipango katika ushauri wa mitume, manabii, wainjilisti, na wachungaji kama wenye nyumba ya mungu iliyejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, Yesu Kristo akiwa jiwe la msingi.

(Mwanzo 2:10-14, Ezek 10:14, Waef 4:11-13, Ufu 4:4-11)

23. Je kanisa la mitume liliendelea baada ya kuanzishwa na Kristo?

*Jibu:* Ndio kitabu cha matendo kama ilivyoandikwa ukuachi na baraka zilizopewa kanisa ikiwa ikiongozwa na roho mtakatifu katika huduma ya mitume.

(Matendo 1:26, 2:41, 2:47, 8:14, 10:47, 23:11)

24. Kwa nini kanisa la mitume walio hai haliendelei?

*Jibu:* Kwa sababu wale katika huduma wa ukuhani walijitakia na hawakuomba bwana kuendelea na huduma na hawakupata ushauri wa bwana kuendelea na huduma wa mtume, ikiwa mahali pa hudumna huo huchukuliwa na huduma uliyefanywa na mwana adamu aliyechukua mahali na utaratibu wa mungu aliyeanzisha.

(2 Wates 2:3-4, Joel 1:1-7, 2 Wakorintho 11:13-15)

25. Matokeo gani alitokea kwa hatua hiyo?

*Jibu:* Kanisa ilipoteza mwelekeo wa roho mtakatifu vipawa niyngi na baraka zilikoma na kanisa iliongozwa na hekima ya mwanadamu na sheria gizani.

(Metha 1:7, Isa 47:1011, Joel 1:13-14, 1 Yoh 5:9)

26. Je mungu alifurahi na tukio hilo?

*Jibu:* la, Yesu Kristo ndiye alfa na omega, mwanzo na mwisho, kulingana na ahadi zake alianzisha kanisa la mitume pamoja na mitume walio hai kutangaza njia ya neema ulimwenguni ili ahadi zake zitimizwe.

(Joel 2:23, Mat 28:20, Yak 5:7)

27. Je jukumu ya mtume kanisani ni ipi?
*Jibu:* Mtume ni mabalozi wa bwana wetu yesu Kristo wanae aminiwa kutoa mafundisho na amri ya Yesu Kristo, na vyombo vinavyotumika na mungu kuwateua wahuduma kutumia vipawa na kuweka muhuri na kutangaza msamaha wa dhambi na nyakati za neema
(Yohana 17:18, Matayo 28:18-20, Wakorinto 5:18-21,
Matendo 6:6-7, Matendo 8:17)

28. Neema ya Kristo ilifanya nini kanisani?
*Jibu:* Neno la mungu kuhubiriwa, msamaha wa dhambi na sacramenti takatifu
(Matayo 26:13, Yohana20:21-23, Matayo28:18-20,Yohana 3:5-8)

29. Sacramenti ya kanisa la mitume ni ngapi?
*Jibu:* Tatu, ubatizo na maji, ushirika mtakatifu na kuwekwa muhuri.
(Matayo 28:19, 26:26-29, Yohana 6:53-54,Waefeso 01:13, 4:30)

30. Kulingana na bibilia mashaidi walio mbinguni ni wangapi?
*Jibu:* Tatu, Baba, Neno (mwana) na roho mtakatifu: na hawa watatu ni mmoja
(1 Yohana5-7, Matayo 3:16-17,1 Petiro 1:2)

31. Kanisa lina mashaidi wangapi duniani?
*Jibu:* Tatu, maji, damu na roho na haya matatu hukubaliana kwa umoja
(lYohana5:8, 5:6, Matendo 10:47, Ufunuol:5,5:9,7:14,22:17)

32. Tunapata nini kwa upatizo wa maji?
*Jibu:* Tumetengwa na ulimwengu kwa ukombozi wa dhambi ya kwanza na kuandikwa ndani ya kitabu cha uzima cha Kristo
(Yohana 3:5, marikol6:16,lwakorinto 12:13, Wagalatia 3:27,
Waefeso 5:26-27, Ufunuo 20:15)

33. Tunapata nini kwa sacramenti ya ushirika mtakatifu?
*Jibu:* Tunapokea msamaha wa dhambi, ili sisi tupate kuwa haki ya Yesu Kristo
(lyohana 1:7, 2 Wakorinto 5:21, Matayo 26:28,Ufunuo 19:8,
2 Petirol:l,lpetiro 2:24)

34. Tunapokea nini katika kuwekwa muhuri mtakatifu?
*Jibu:* Ubako wa roho mtakatifu.
(Matayo 3:16-17, 1 Wakorinto12:13, Warumi 6:3-4,Yohana 14:17,
Waefeso 4:30)

35. Kwa nini mungu ametupatia upako wa roho mtakatifu kwa kuwekwa muhuri?
*Jibu:* Roho huwa ndani unatuandaa tuwe kama mfano wa Kristo na kuwa tayari chiandaa kwa kuzaliwa mara ya pili tuwe kama bwana wetu atakaporudi duniani
(Warumi 8:14-16,1 Wakorinto 6:9-20,2 Wakorinto 3:18, lwatesoloniki)

36. Mbona tunaamini kwamba Bwana Yesu Kristo atarudi karibuni?
*Jibu:* Kwa sababu ishara zimeonekana nyakati hizi kama ilivyonenwa na Bwana wetu na manabii, na kwamba mbele za mungu miaka elfu moja ni kama siku moja kulingana na bibilia takatifu
(Matayo 24, Matendo 1:11, Waiberania 9:28, Ufunuo 3:11, 2 Petiro 3:8)

37. Matukio gani katika ulimwengu kabla Kristo kurudi?
*Jibu:* Kulingana na bibilia takatifu, kanisa la mitume litakuwa na dhiki kuu na mateso, na wenye mamlaka watainuka kuitawala dunia kulingana na njia za kishetani na watakuwa na nguvu juu ya mwana adamu na kuwaamuru wasimwabudu mungu au Kristo
(Ufunuo 13:6-8, 13:16-17, 13:13-14, Matayo 24:21-22,)

38. Tutafanya nini wakati huo?
*Jibu:* Lazima tupitie mateso yote na majaribu na tusiungane na ulimwengu, lakini tusimame imara kwa imani yetu katika Kristo kwa kumwamini Bwana
(Matayo 24:13, 10:22, Yakobo 1:12, Isaya 26:4, 1 Petiro 1:7-9)

39. Kutakuwa na tuzo kwa uaminifu huu?
*Jibu:* Mungu atatupatia nguvu na bwana wetu Yesu Kristo atakaporudi wale waumini katika Kristo wataepuka mauti
(Isaya 26:8, Luka 20:36, Isaya 25:8,1 Wakorinto 15:24, 2 Timoteo 1:10)

40. Kurudi kwa Yesu Kristo kutakuwa na lengo gani?
*Jibu:* Atatumwa kutoka mbinguni kama bwana arusi, akizileta roho zote kutoka madhabahu ya dhahabu na paradise, kufufua miili yao kutoka arthini kuzaliwa upya, kuwatimizia waumini walio hai na kupokea kanisa lililochiandaa kama bi arusi kulipatia baba katika ndoa ya bwana mbinguni.
(2Wateseloniki 4:13-17,2Timoteo 4:8, Ufunuo 21:2, 2 Wakorinto 11:2,)

41. Ni nini kitatokea duniani wakati huu wa baraka mbinguni?
*Jibu:* Dunia na yote yaliyomo itafanywa upya na yote yafanywe mapya
(2 Petiro 3:6-7, Daniel 2:44, Isaya 11:1-9, Ufunuo 3:12)

42. Je tutabaki na Yesu mbinguni?
*Jibu:* La, atarudi duniani pamoja na watakatifu wote walie shiriki katika ushindi wake, amfunge shetani, na kuanza ufalme, (milinia) utawala wa amani kwa miaka elfu moja (1000)

(Ufunuo 20:1-4, Isaya 65:17, 66:22, 2Petiro 3:13)

43. Karibu na mwisho wa ufalme huo tukio lipi litakalo tokea?
*Jibu:* Shetani atafunguliwa kwa mda mfupi kuwajaribu wote waliozaliwa katika nyakati za ufalme huo

(Ufunuo 20:7-8,)

44. Shetani ataenda wapi?
*Jibu:* Mungu atamtuma malaika kumshinda shetani na wafuasi wake, na kuwekwa kuzimuni kuongojea hukumu.

(Ufunuo 20:9-10)

45. Baada ya utawala wa amani wa miaka elfu moja (1000) kutakuwa nini?
*Jibu:* Ufufuko wa pili wakati wote kutoka mwanzo wa dunia watasimama ili wapate hukumu wa mungu

( Ufunuo 20:11-15)

46. Mwelekeo wa mwisho wa kanisa aminifu ni ipi?
*Jibu:* Uzima wa milele mbinguni katika utukufu wa mungu.

(Ufunuo 22:5, Matayo 13:43, Waifilipi 3:21, Zaburi 73:24,)

47. Majina kamili za silaha zinazotakikanana Bi arusi wa Kristo:
i) Kamba ya ukweli
ii) Kuvaa dirii ya haki kifuani
iii) Kufungwa (viatu) miguu kwa injili ya amani
iv) Ngao ya imani
v) Chapeo ya wokovu
vi) Upanga wa roho
vii) Sala zote na maombi kila wakati

(Waefeso 6:13-18)

---

# MAOMBI
(Prayers)

Kila siku inatupasa kumwomba bwana kristo tukiwa duniani tukiweka mfano, kila husubuhi mchanana usiku tukisukuru pia na nyakati za shida.

**Watesilonike 1 5:17-18**
Sali wakati na muwe na shukrani katika kila hali. Hayo ndiyo anayotaka mungu kwenu kuungana kwenu na kristo yesu.

**Mathayo 26:41**
Kesheni na kusali hili msije mkaingia katika majaribu. Roho inataka lakini mwili ni dhahifu

Yafuatayo ni mwongozo wa maombi ya kila siku:

# MAOMBI YA BWANA

(The Lord's Prayer)

Baba yetu aliye mbinguni,
Jina lako litukuzwe,
Ufalme wako uje.
Mapenzi yako yatimizwe,
hapa duniani kama huko mbinguni.
Utupe leo riziki yetu.
Utusamehe deni zetu,
kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.
Na usitutie majaribuni,
lakini utuokoe na yule mwovu.
(kwa kuwa ufalme ni wako,
na nguvu, na utukufu,
hata milele. Amina)

*Swali:* neno amina lina maana gani?
*Jibu:* neno Amina maana yake, "yesu, bwana iwe ifo"

# MAOMBI YA WATOTO

(Children's Prayers)

Ina wapasa watoto wafundiswe kuomba wakiwa wachanga,na yafuatayo ni maongozi ya maombi ya watoto

# MAOMBI KWA WATOTO BAADA YA SHARA KWAI CHAKULA

(Aprayer for the children after Grace has been said for meals)

Tunashukuru ewe Bwana kwa baraka katika upendo wako wa kila siku. Ewe Mungu tupatie neema na huruma hadi mwisho. Katika Bwana na Mwokozi wetu Yesu kristo.

Amina

# MAOMBI YA HASUBUHI KWA WATOTO WADOGO

(Morning prayer for little children)

Baba mpendwa nimeamuka,
kutoka mapumusikoni ya usingizi mwema,
mapenzi yako yawe matumaini yangu,
na juu ya njia nyembamba.
Malaika wakae nami katika Bwana na Mwokozi wetu Yesu kristo. Amina

# MAOMBI YA JIONI KWA WATOTO

(Evening prayer for little children)

Mungu mpendwa ninakupa shukurani kwa kila jambo,
afya ulinzi,
chakula na nuru katika siku hii hadi usiku,
ninapo lala.
Tulindwe na malaika wako katika Bwana na Mwokozi wetu Yesu christo.
Amina

# WATOTO BAADA YA USHILIKA MTAKATIFU

(Children after Holy Communion)

Bwana nashukuru kwa siku hii,
uniongoze kwa njia zako,
neema yako ikae nami kutokana na dhambi niwe huru;
uwaweke malaika wako karibu nami kila siku,
hili nisiogope kamwe katika Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Amina

# WATOTO WAKIINGIA KANISANI

(Children entering church)

Roho mtakatifu,
uzuri na wema,
nifundishe kilijo chema:
uwe nami katika siku hii,
sasa nina chinyenyekea kwa maombi.
Bariki mitume wetu na upendo wako,
wachaze na hekima kutoka juu katika Bwana Mwokozi wetuYesu kristo.
Amina

# MAOMBI YA WATOTO KWA WA ZAZI WAO WALIO WA MUNGU

(A prayer for children for their Godly parents)

Baba wetu wa mbinguni, nakushukuru kwa hulinzi na maombi ya kila siku kwa wazazi wangu. Ninaomba, Bwana mungu, kwa kutuma mwongozo na kuitawala Roho yangu, ili imani ya ukweli ya wazazi, ikae ndani yangu pia.Ewe mungu nisaidie uweke mbele yangu huduma na tabia kamili, ambaye walitia,moyoni mwangu. nisaidie baba wa upendo kwa kufanya siku zao sing'ae kama jua lotuapo hili maisha na imani iwe jibu linalohishi kwa maombi yao: na wakati ninaomboleza kama yule anaomboleza kwa wazazi, kumbukumbumbu zao siwe nami,kama nyota inaoang anza, ili iniongoze kwa safari yangu kwa siku njema na siku mbaya yamaisha yangu nimalise safari yangu. Ewe bwana jali maombi yangu nyenyekevu katika tendo kuu ya upendo katika kristo Yesu.

Amina

# TAFSIRI YA MFANO WA 4H

(definition of the 4R emblem)

~ Mfano uanza na + ambaye uonyesha msalaba wa yesu kristo mahali imani yetu uazia (The emblem with a cross which signifies the cross of Jesus Christ where our faith begins.)

~ Ifuatayo ni mvilingo
Msalaba ambaye unaonyesha imaini yetu ambaye inayozunguka na hauna mwisho -Yeye ni mwazo na mwizo wa imani yetu. (The next item is a continuous circle around the cross which signifies our whole faith which revolves around Jesus Christ and is never ending - He is the beginning and the ending of our faith.) ⊕

~ mfano wa 4H (4R) Uonyesha (The 4R's then take shape signifying:-)

**Haki katika mawazo,** (Righteousness in Thoughts,)
**Haki katika maneno,** (Righteousness in Words,)
**Haki katika matendo,** (Righteousness in Deeds,)
**Haki katika njia zote.** (Righteousness in Ways,)

Ufupi wa haya 4 kama

**HAKI ~ KIFALME ~ WEMA ~ UTAJILI**
**(Right ~ Royal ~ Righteous ~ Rich)**

1. Lasima tujitahidi kuishi maisha ya haki kulingana na Biblia takatifu.
2. Lazima tujitahidi tuwe waminifu katika ufalme kama bibi arusi ili tuwe na ushirika na Kristo Mfalme.
3. Tutakuwa tu wenye haki katika ushirika wa mwili na damu ya Kristo.
4. Kila siku sisi nimatajiri katika ahadi Kristo aliye wapatia Mitume wake na katika neno la Mtume walio mwamini yeye.

# MAANA YA UTHIBITISHO
(The meaning of confirmation)

Tuta yachukwa madaraka ya nadhiri ya upatizo iliyo pewa na wazazi mbele ya Bwana kwa niaaba yetu tukipatizwa.

# NYIMBO ZA UTHIBITISHO
(Confirmation Hymns)

### 95. Birikani
Melody No. 16

1. Birikani nadhiri yangu iliyo nenwa
kwa wazazi wangu katika Bwana.
Madhabahuni na kumbuka Ewe
Mungu wangu, Umeniongoza
Tangu nilikuwa wako,
Umenifundisha kwa kunijalia
Nitahishi na wewe tu.

2. Bwana kutana nami na wokofu wako
Katika agize la kanisa lako.
Nionekane kwa uthibitisho wako,
Kwa upendo na ukweli wako hivi leo.
Nifuate njia zako zote
Nita amini ilinzi wako
Na nita kufuata na njia zako.

3. Mwokozi na pumziko, katika sifa njema
Uwezo katika neon la roho
katika mwaliko nita rithi
Ahadi zako za furaha, E Bwana sasa na daima,
Naishi katika uaminifu wa kweli.
Uwezo na imara na nguvu ya usindi
Tumaini katika hatari na furaha katika huzoni.

## 166. Ewe ndugu safari ya maisha yaanza

Melody sankey 699.

1. Ewe ndugu safari ya maisha ya anza.
Na uhodari nasimama imara
Tazama mwendo ambaye umechagua
Kuwa mwenye bidii, mwangalifu, na hekima!
Kumbuka - mbili ziko mbele yako na pia nataka uangalifu
Lakini moja uongoza katika upotevu
Mwingine katika furaha na kupendeza sana

Chorus(wimbo)

Mungu nisaidie nifuate pendera yake,
Na kumtumikia popote uendapo
na uki jaribiwa, ndugu,
Mungu atakupa neema ya kusema "la".

2. Ewe dada, usijitoe kwa ibilisi
Ingawa wengine wanayafanya,
Simama imara katika uwezo wa Bwana,
Kuwa mtiifu, mwaminifu na kila jaribu litakufanya uwe na nguvu,
Ikiwa, katika jina la Bwana,
Pigana kwa hodari chini ya viongozi wako
Ukisikia sauti ya neno lake.

Chorus(wimbo)

3. Ewe ndugu, mwokozi anaita
jihadhali na hatari za dhambi
usipinge sauti ya roho mtakatifu ambaye uong'oneza ndani kwa upole
Mungu akuita uingie kwa huduma,
tuishi kwake hapa,
siku kwa siku
nashiriki katika utukufu ambaye autatoweka.

Chorus(wimbo)

# UONGOZI KATIKA MAOMBI KWA WASHIRIKI

(Guideline to prayers for members)

Kila asubuhi watu wa nyumbani inatupasa tuungane kwa kuita utatu wa Mungu na kusoma andiko kutoka Biblia takatifu. Yatupasa maombi yatolewe pamoja na mwongozo.

A prayer should be offered along the lines of the guide:

# MAOMBI YA ASUBUHI

(Morning prayer)

Katika jina la Mungu Baba, Mwana na Roho mtakatifu. Bwana Mungu, tunainama chini katika unyenyekevu mbele zako na kuleta shukrani kwako, kwa kutulinda kutokana na madhara wakati wa usiku na kutupatia baraka zako.
Bariki tukiondoka asubuhi hii hili jioni tukusifu, na tufurahi kwa matendo yako ya upendo kwa siku nzima, ulinzi wa malaika katika siku hii na utuweke mbali na majaribu,. Taabu, Ugonjwa, Huzuni Ajali, Lakini kuliko wote kifo cha mapema, dhamira na matendo yake matakatifu na yenye faida, baraka na bila hatia ili siku ikiiza tuwe katika upande wako na pumziko katika tumaini takatifu ili wema na baraka iwe nazi. Linda mitume na wajase na nuru na hekima ya roho mtakatifu. Linda kanisa na watumishi wakati wote, mkono wako uongoze kazi ili ongezeko liweke wakf. Wako.

**SALAMU YA ASUBUHI** (Morning Salute)

Tunaomba Roho uende kwa wale wanao kuita katika siku hii. Linda Rais na Serikali yake na utupatie haki na amani ya heshima katika nchi yote. Jalia maombi haya katika Bwana wetu na Mwokozi Yesu kristo.

**Neema ya Bwana na Mwokozi yesu kristo, upendo wa Mungu** Baba, na ushirika wa Roho Mtakatifu uwe nazi zote.
Amina.

---

Yatupasa tuseme Sala (neema) kabla ya kila mlo kama ifuatayo:

# NEEMA - OMBI MEZANI KABLA YA KULA MLO

(A prayer at table before taking meals)

Baba wa mbinguni tuna kushukuru kwa unyenyekevu kwa sawadi ambayo umetubariki, tunaomba ubariki tukila chakula hii kwa mwili, katika Mwokozi wetu Yesu Kristo.
Amina.

Yatupasa watoto waombe kabla ya sara kama ifuatavyo:

Ikiwa pahali pa maombi haifai kuomba sala zote kwa sauti, basi maombi yafanywe kimya na kwa ufupi kwa mfano :

"Bwana bariki Mlo huu." Amina

Wakati mwingine usiku ama jioni, wakati watu wa nyumba wakiwa pamoja inawapasa waongoje kidogo na kusoma zaburi ama mithali kutoka Biblia takatifu. Ombi la jioni yapasa isemwe na wenye nyumba kabla kuenda kulala.

# MAOMBI YA JIONI

(Evening prayer)

Tena ewe Bwana Mungu, katika unyenyekevu na moyo wa masikitiko na roho wa toba, tumekuja mbele yako baada ya siku kuisha na kushukuru, sifa, heshima na utukufu kwako, kwamba una upendo wako, utulinde kutokana na majaribu,taabu, magonjwa, huzuni majonzi na ajari katika siku azima. Tunaingia usiku na atujui We lilo mbele yetu lakini Bwana, Tuna kusihii kwa unyenyekevu uweke ulinzi wa Malaika pande zote na nyumba za watu wako, tafafhali tupatie pumziko la kulala ili tuamke asubuhi tukiwa tumeburudika kutoka mapumziko ili tuyatimize mengi kaatika kazi zetu za kila siku.

Ulinde kanisa lako na watumishi wako, uwafunike mitume na hekima na ufahamu wa Roho Mtaikatifu na wapate afya na nguvu kutimisha mwito wao, uwalinde vijana wa kanisa kutoka kwa majaribu na mkono wako ili uwaongoze kwa kazi ili ongezeko liwekwe kwako. Linda Rais na serikali yake na amani ya heshima itawale kati ya nchii yote. Ikiwa tumefanya dhambi katika siku hii, tunaomba dhambi hizi zifuniikwe kwa neema iliyoletwa kwetu na Bwana wetu na Mwokozi Jesu Kristo. Amina. Neema ya Bwana na Mwokozi Yesu Kristo.

Amina.

Neema ya Bwana na Mwokozi Yesu Kristo upendo wa Mungu Baba na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae ndani yetu zote.

Amina.

# MAOMBI MENGINE

(Other prayers)

Tukiingia kwenye ibada, maombi yapasa yatoke ndani ya moyo. Yafuatayo ni mwongozo tu.

# MAOMBI KWA WASHIRIKI WAKINGIA KWA IBADA

(Prayer for members entering for divine worship)

Bwana Mungu, nakushukuru kwa kuniruhusu niingie katika ibada, nakusihi Roho Mtakatifu atawale dhamira yangu nitii kwa kuhubiri injiri na kuyaweka moyoni mwangu. Baba mupendwa, nakusihi uwape watume wako na watumishi wako na uwaongoze kwa Roho Mtakatifu watangaze ujumbe wa injiri kwa ustawi wa moyo wangu. Amina

# MAOMBI BAADA YA USHIRIKA MTAKATIFU

(Prayer after partaking of the Lord's Supper)

Baba Mpendwa, nina kusihi kwa unyenyekevu nipate haki iliyo ndani ya mwili mtakakatifu na damu ya Yesu Kristo yaliye andaliwa kwangu na Roho Mtakatifu uliyetumwa na Bwana ambaye nimeshiriki. Nakusihi upeleke baraka kwa Wagonjwa na walio dhurumiwa na wale wasio hapa na wale wamewekwa amana chini ya uangalifu wangu. Amina.

# MAOMBI KWA WALE WALIO GEREZANI KWA MSAMAHA

(Penitential prayer asking for forgiveness)

Ewe Mungu wa haki, utuongozaye tuwe wapole katika Roho Mtakatifu na kuturudisha tuwe wanyenyekevu na watulivu kwa njia, utuzamehe dhambi zetu na makosa ya hali yetu ya maombile. Ewe Bwana ukubali na ukumbuke huruma na wema, tusamehe dhambi zetu na tuokoe kutokana na adui na shida zetu na utupatie neema. Utuweke katika ukamilifu na shughuli za haki, ili tukae, uhuru kutoka kwa shida na tuwe salama kwa maadui wetu. Ewe Mungu tupatie haja ya maombi katika Yesu Kristo ambaye Yeye ni Mungu nawe. Amina.

# MAOMBI KWA FURAHA KATIKA NDOA

(A prayer for happiness in marriage)

Ewe Bwana Mungu, tubariki na kila siku tufanye tuwe na raha katika maisha yetu ya ndoa. Ufungie masikio yako kwa maombi yetu, tupatie tunakusihi, kwa moyo wa masikitiko na Roho wa unyenyekevu. Tupatie moyo wa Jina lako takatifu ili tufanye yaliyo mema ukiwa tayari na Roho ya kukata shauri ili tulete shida zetu zote tunayekutana. Kwa upendo wako neema na rehema utukinge tusianguke

shimoni katika maisha ya ndoa ili, katika wakati wa maisha yetu tuonekane na tuonje wema wako Ewe Bwana rehema yako yakupendeza iwe nanga kwa roho zote milele. Tupatie moyo wa Roho Mtakatifu utufanye tufurahie nguvu za uumbaji na za utukufu wa Ufalme wako. Tupatie ushujaa kunyenyekea sisi kwa sisi ili tuwasaheme kabla ya jua lituapo. Ewe Bwana Roho Mtakatifu uwe wakiri katika nyumba yetu ili furaha na radhi itawale. Tuongoze katika Roho Mtakatifu Uongoze maisha yetu yanaye kupendeza mbele yako. Amina

# MAOMBI YA KUTUINUA

(Prayer to uplift us)

Bwana ndiye Mchungaji wangu
sitapungukiwa na kitu
Katika malisho ya majani mabichi hunilaza
kando ya maji ya utulivu huniongoza.
Hunihuisha nafzi yangu; na kuniongoza
Katika njia za haki kwa ajili ya Jina lake
Naam, nijapopita kati ya ponde la uvuli wa mauti,
sitaogopa mabaya;
Kwa maana Wewe upo pamoja nami,
Gongo lako na fimbo fyanifariji.
Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi
wangu
Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe
changu kinafurika,
Hakuna wema na fadhili zitanifuata.
Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani
Mwa Bwana Milele

# BARAKA ZA MTUME

(Apostle blessing)

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo
Upendo wa Mungu Baba
Ushirika wa Roho Mtakatifu
Iwe nasi sasa na milele.

Amina